
Hauko
peke
yako
Sehemu za kitabu

Madondoo toka kitabu cha Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu:

En couple et pourtant seul ?
Seul à un âge avancé ? Vivre dans l'unité !
Tu n'es pas seul – Dieu est avec toi

Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Kumpata Mungu! Wapi? Na Vipi?
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Mafundisho ya Yesu Mlimani
- Mnaishi milele. Hakuna mauti
- Yesu na wanyama
- Hili ni Neno Langu A na Ω
- Uwezekano wa kuzaliwa upya katika mwili wa mwanadamu ni neema ya Uzima



First Edition in Swahili: March 2023
1ère édition en Swahili: Mars 2023

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Nguvu, upendo na hekima ya ulimwenguni pote ya Mungu inaunda sumaku kubwa yenye mvuto ambao unahitaji kuvuta kwake, kila mmoja wetu. Tukikubali kuvutwa, mvuto huo utaimarisha mawasiliano na utu wetu wa ndani ambamo mna nguvu asilia, uwezo wa uwepo wetu wa milele unaongoja kuwekwa huru. Hayo yanajidokeza ndani mwetu kama hisia, aina ya majonzi, nuru kubwa inayotuinua na kutujaza.

Kwa hiyo, ni wajibu wetu kupiga hatua ya kwanza kwenda kulaki nuru ya Mungu inayotungoja hadi muda tutakapoamua kugeukia ndani mwetu na kujielekeza daima upande wa chemchemi ya milele, yaani Mungu. Vipi? Kwa kufanya mazoezi ya kujikataa sisi wenyewe na kuingia katika mazingatio makubwa ndani mwetu, kuzama katika ukimya wa ndani na maombi. Kuomba kunamaanisha kujitahidi kuwasiliana na Mungu, na Kristo ndani mwako wewe mwenyewe.

Baaadhi ya watu hutumia maisha yao yote kwa kutafuta upendo, furaha, ulinzi, na mahali ambapo wanajihisi wenye raha na salama. Licha ya kukutana na watu wengi maishani mwao, licha ya «uhusiano» wa kimapenzi na ndoa kadhaa, baadhi yao wanakiri, katika umri fulani, kwamba hawajafanikiwa kamwe na wanakubali kuwa wanaishi katika upweke au kutengwa.

Baaadhi ya watu hutafuta kwa wengine sifa ambazo hawana ndani mwao wao wenyewe. Wanayatia matamanio yao yote kwenye hali za mtu fulani, wakidhani kwamba wamefikia lengo lao kupitia mtu huyo ambaye kwao ndiye kigezo kuhusu ubora wa mambo. Kwa kweli, mtu huvuta tu kwake kile alicho yeye mwenyewe bali sio kile anachotamani. Kwani daima vitu vinavyofanana, hujikusanya pamoja.

Kuishi maisha ya uadilifu katika ujana kunamwezesha mtu mzee kufa kwa hali ya uadilifu.

Hata kama nyakati zinakimbia na kubadili hali ya mambo, hakuna mwanadamu atakayeweza kudai kwamba amefikia raha ya kweli, raha ya kudumu. Ulimwenguni humu, hatuwezi kamwe kufikia hayo. Kwa sababu sisi si wenyeji wa ulimwengu huu! Yesu, Kristo, alituambia jambo kama hili: «*Ufalme wa Mungu umo ndani mwenu*», alisisitiza tena: «*Tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake na mengine yote mtayapewa kwa ziada.*»

Mtu ambaye, muda wa maisha yake duniani, pa wakati, ana dhamiri ya maneno hayo yanayotoka kwa Roho na anayeongoza maisha yake kulingana na maelekezo hayo, hatakuwa kamwe mpweke, hata katika uzee sana, ikiwa kwa mfano mkewe au wanaye hawapo tena. Maisha yake yatakuwa yamepata maana yake yote kwa sababu atakuwa amejifunza, pa wakati, jinsi ya kuufikia Ufalme wa Mungu, kufikia Roho wa Baba yetu wa Milele aliye ndani mwetu. Uzee wa maisha yake utajaa upendo, hekima na usalama.

Mtu anayempenda Mungu kwa moyo wake wote hayuko kamwe peke yake.

Tufahamu daima kwamba Ufalme wa Mungu, uzima wa milele, ndiyo nchi yetu daima damana. Tayari, katika vazi hili la kidunia, yaani mwili, tunaweza kuikaribia nchi hiyo ili hatimaye tufikie lengo la maisha, ambalo ni kurudi maskani, kwenye nchi yetu ya asili ambayo ni ufalme wa ndani, ufalme wa ukimya na amani, ufalme wa maisha ya kiroho.

Tunapolenga uzima wenye thamani kubwa, uzima wa kiroho, nafsi yetu huamka, nayo inaamsha urithi wetu wa kimungu na tena inafunua ndani mwetu sisi wenyewe uzima wa milele, uzima usiokufa. Mipapatiko ya utu wetu wa ndani inaimarisha majonzi ya nchi, angaiko hiyo ya moyo ambayo mara nyingi mtu huelewa vibaya na inayomwelekeza kwenye maisha ya nje, kwenye hisi.

Tamaa hiyo isiyotosheka, kumbukumbu hiyo ya nchi isiyoweza kuelezeka si kitu kingine bali dhana kwamba kuna mazingira

salama, ya amani na raha. Ndiyo maana mwanadamu hana pumziko, hana utulivu, anatafuta na kutafuta tena.

Ni utafiti, matamanio ya kitu ambacho hatuwezi kuelewa kwa undani kwa sababu tumekipa majina kama vile «mume», «mke», «utajiri», «pesa», «afya», «bidhaa», «anasa», na kadhalika... Kwa kweli, sababu ya utafiti huo ni ya kina sana: Tunatafuta kupata asili yetu, kina cha mioyo yetu, nchi yetu ya milele.

Mwanadamu atabaki bila utulivu wakati wote ule ambao nafsi yake haitarudi upya katika bahari kubwa ya uzima, Mungu, upendo mkuu na umoja. Mtu na nafsi yake wataendelea kutafuta hadi muda ambapo wote wawili watakapopata upendo halisi wa Mungu, Baba wa Milele wa nafsi zote na watu wote. Utafiti huo hukoma hadi muda ambapo mtu atakapopata nchi yake ya asili kwa Mungu ambaye ni umoja ulio katika

watu wote, katika viumbe vyote vilivyo hai na aina zote za viumbe.

Unajifunza kwa kuacha kufanya kama wale wote ambao hawafikirii juu ya kile kinachowatokea na kuwapata. Swali hisia zinazojitokeza ndani mwako. Zama ndani ya nguvu ya uzima inayotiririka ndani mwako na ungana na kituo cha nne cha nguvu kinachopapatika karibu na moyo wako ili kuomba msaada. Nguvu ya nuru inayomulika sana katika kituo hicho cha dhamiri ni nguvu ya Kristo wa Mungu, nguvu ya nuru ambayo inasaidia na kuponya.

Kila hatua kuelekea Mungu inakuruhusu kuelewa kwa kina sana matukio yanayokuja kwako kukuathiri. Kila siku ya maisha yako katika hali nyingi, hekima isiyo ya ulimwengu huu inakuonyesha njia. Hauko peke yako.



Kila mchana unakutaarifu kupitia matukio mengi, madogo kama vile makubwa. Kwa hiyo una nafasi nyingi za mazungumzo na Mungu. Anakusikia. Wazo unaloelekeza kwake, neno la kirafiki, msaada kwa jirani yako, vyote ni njia ya kuwasiliana na Mungu.

Kila kitu tunachokiona, na pia kile tusichokiona, ni nguvu. Hakuna nguvu inayopotea. Kila mwanadamu anawakilisha jumla ya nguvu. Kila mnyama ni nguvu. Mazingira yote, hadi ua ndogo lisilo na maana, ni nguvu. Kila madini ni nguvu na ina uzima unaotoka kwa Mungu. Uzima ni nguvu.

Una uzima ndani mwako. Viumbe vya mazingira ni zawadi kutoka kwa Muumba wa watu wote. Pumzi ya Mungu pia imo ndani ya wanyama. Ni nguvu ya uzima ambayo tunaweza kuhisi ndani ya maumbile yote.



*N*enda ukamlaki Mungu, ukimya wa milele...

Kwa mfano, katika matembezi yako ndani ya mazingira, tembea kwa uangalifu. Simama mara kwa mara na acha macho yako yatazame mashamba, makonde na misitu. Jua kwamba katika kila jambo, Mungu huja kukutana nawe. Acha mazingira yaguse moyo wako. Uwe mwenyewe tayari kupokea misukumo kutoka mazingira inayotaka kugusa moyo wako au utu wako wa ndani.

Ndani ya mti, ua, jani, ndani ya shamba la ngano, ndani ya ndege hata pia ndani ya paka mdogo, mna uzima. Na uzima upo hai! Uzima ni dhamiri. Upo katika mawasiliano. Uzima unatoa na kupokea. Nini? Hali za dhamiri, nguvu bora, mikondo ya hisia ambayo tunaweza kuziita misukumo. Kwa hivo, ndani ya dhamiri yetu inayogeuka tulivu, ndani mwetu wenyewe, tunaweza kuhisi misukumo ya uzima. Kwa hiyo uzima unazungumza nasi kupitia mti, ua, kupitia jani au kupitia shamba la ngano, kupitia ardhi, kupitia

ndege, paka mdogo, nyota ya angani. Ni Roho wa uzima, Mungu, anayesema nasi.

Kwa kuhisi misukumo inayotolewa na ulimwengu wa asili, ni muhimu kusitisha fikra zetu zenye kujaa machafuko na kutuliza hisia zetu. Tunaweza kujifunza, kujizoeza kupata utulivu na ukimya ndani yetu wenyewe.

Upendo wa kweli ndiyo nguvu ya msingi inayounga viumbe vyote na vitu vyote. Kwa hiyo upendo wa kweli ni nguvu ya mbinguni. Umo ndani ya kila mwanadamu, ndani ya kila kiumbe, ndani ya mambo ya asili, ndani ya kila kitu tunachokiona na vilevile ndani ya kile kisichoonekana kwa macho yetu.

Jifunze kutazama na utajitambua, utamjua jirani yako. Jifunze kusikia na kutambua mambo yanayotendeka ndani mwako na utajua kuelewa. Jifunze kuwa na mtazamo wa ndani wa mambo na utaishi vema siku zako. Jifunze kusikiliza ujumbe wa maumivu

na huzuni. Daima ujumbe huo unakuonyesha njia ya maisha bora na ya juu zaidi.

Upendo halisi hutuweka huru. Haujui kutengwa. Upendo halisi, yaani Mungu, upo siku zote.

Upendo unaupa moyo mazoea mazuri kwa kuacha akili ijadili na kutathmini mambo kwa mujibu wa upendo.

Upendo husamehe na daima unapata njia ya uaminifu.

Upendo unajua kusubiri ili kutoa kwa muda muafaka.

Upendo humwacha jirani awe huru bila kumtelekeza.

Upendo unamuachia nafasi jirani moyoni bila kujali tabia yake.

Upendo ni neema ya moyo inayojidhihirisha ndani ya jirani yangu.

Upendo wa Mungu unamaanisha kutafuta kila siku kuelewa ni nini mapenzi ya Mungu na kuelewa jinsi ya kuyatimiza.

Ni vipi kujifunza kupenda:

Anzia kwenye kikundi kidogo, kwenye familia yako, kwenye watu wachache wa karibu nawe. Jizoeze kumwelewa jirani yako. Msikilize bila kumkata kauli kupitia maelezo yako. Hivyo, utatambua kwamba pengine jirani yupo tofauti kidogo na jinsi ulivyokuwa unamfikiria na kwamba naye pia anakabiliana na hali kama na zako. Ikiwa anahitaji msaada, ikiwa hafaulu katika mambo fulani, msaadie, bila kutarajia asante au shukrani kutoka kwake. Hizo ni hatua ndogo, zenye umuhimu mkubwa, zinazotuongoza kwenye upendo wa Mungu na wa jirani.

Kupenda hakumaanishi kupenda na kuridhia ukiukaji wa maadili wa mwanadamu, kukubali dhambi ya jirani, bali ni kupenda na kuthibitisha mema ndani mwake, kuthibitisha Mungu. Kuelewa mafundisho hayo ya juu sana ya Yesu, Kristo, na kuifanya kuwa kigezo cha maisha yetu kunahitaji mafunzo na kufanya mazoezi.

Upendo halisi ni nguvu ya ukombozi isiyomtia jirani chini ya himaya yetu, bali, tofauti na hayo, inamuacha huru.

Acha maneno haya yafanye kazi ndani mwako: upendo wa Mungu ndani mwako ni mkuu mno kupita kiasi unachoweza kufikiria au kuelewa.

Jifunze na kujizoeza kila siku dhamirini mwako kuwa Mungu yu ndani mwako. Sitisha kwa muda mara kadhaa kwa siku shughuli zako na tamka sentensi kwa moyo wote: Mungu yumo ndani mwangu.

Jifunze na kujizoeza kutambua utu wako halisi, ukijua kwamba ndani mwako mna uzima wa milele. Hauko peke yako.

Ni jambo linalowaletea raha na furaha majirani zako ndilo tu linalokufanya uwe na raha ya kweli na ya kudumu.

Tunapozungumzia kuhusu Mungu, maswali yanayoulizwa mara nyingi ni:

«Mungu yuko wapi? Je, anajificha? Kwa nini anajificha? Kuwepo kwake kunatiliwa shaka. Mungu yuko kila mahali. Kwa hiyo «anaonekana», anapatikana kutokana na uzoefu wa kila mtu kuhusu Mungu. Mungu haonekani kwa wanadamu muda wote ule anapojitenga na nuru au uzima ambao ni Mungu.

Watu wengi hupoteza imani kwa Mungu kwa sababu wanachanganya Mungu na suala la Kanisa. Iwapo mwanadamu haamini kuwepo kwa Mungu, basi mtu huyo anakosa imani na baada ya muda anakuwa mtu asiye na msimamo, kama mtu anayetangatanga.

Mtu asiyepuuza bali anayejitahidi kujifunza kutokana na matukio ya maisha ni mwake na kufikia maendeleo ya kiroho inayohitajika, kwa kweli anaanza kuishi. Maisha halisi yanamjaza mtu na kumfanya awe mwenye raha.

Usisahau: jambo unalohisi, unalolifikiria na kunena na linalozusha hisia ndani mwako, lina ujumbe kwa ajili yako. Tathmini hisia zako na utajitambua vizuri sana. Hatua kwa hatua, utageuka mwamuzi wako wewe mwenyewe. Utahisi ndani mwako, na baadaye, ndani ya mwenzio, mambo ambayo bado hujawahi kuhisi.

Usife moyo ikiwa, kutokana na maamzi yako mazuri, mambo mengi yenye shinikizo yatajitokeza kwako mwanzoni. Ni kawaida kabisa. Usikate tamaa!

Jiswali ni tangu lini una tabia kama hizo na utaelewa kuwa tabia hizo hazitakoma mara moja.

Uzima unachanua ndani mwako. Ng'oa ua la upendo lililo ndani mwako na utanukia manukato yake.

Jifunze kuwa mtulivu katika misukosuko ya wakati huu. Pangilia siku zako ili uweze kuchukua muda mfupi kabla ya kushughu-

likia tatizo fulani, kabla ya mazungumzo muhimu, kabla ya kila hali, ili kufikia utulivu na mazingatio ya ndani itakayokuwezesha kubaini katika hali hizo jambo lililo muhimu na lile lisilo la muhimu.

Mungu ndiye nguvu ya ulimwenguni kote. Mungu yuko karibu sana nasi kuliko mikono na miguu yetu. Kwa hiyo Mungu yumo ndani ya nafsi na kila seli yetu. Yumo ndani ya mishipa na kila sehemu ya mwili wetu. Mara nyingi swali hili la kufahamu jinsi Mungu, nguvu ya ulimwenguni kote hufikia mwilini mwetu linaulizwa. Mtu aliyechota ujuzi wake wa kiroho kwenye chanzo cha milele, atajibu: «Kupitia pumzi, kwani pumzi ni uzima.»

Maombi ya kutafakari ni chanzo cha nguvu na nuru. Kuna uwezekano kwamba sala ya mazingatio igeuke sala kwa ajili ya jirani yetu, kwa ajili ya viumbe tofauti vya umoja mkuu vinavyotugusa moyoni, mazingira, wanyama na vitu vingine vingi. Aina hiyo

ya maombi yanatujaza na kutuleta karibu na Mungu, hasa iwapo maishani mwetu tunayatimiza na tena maombi yetu yanajidhihirisha katika mwenendo wetu. «Mazungumzo» kama hayo, mawasiliano kama hayo na Mungu mara nyingi huambatana na hisia ya kuridhika na shukrani...

*M*tu ambaye amepata utu wake halisi kwa kujitahidi kila siku kufikia lengo la kuugundua, hayuko peke yake. Amefikia lengo lake na hayo yanamfurahisha sana.

*M*ungu ni yote katika kila kitu. Pia anataka kuwa yote katika kila kitu kwa ajili yako. Anakungoja. Wapi? Ndani mwako!





Roho huru – Mungu ndani mwetu

Kitabu hiki kinamwelekeza msomaji kwenye njia ya uhuru na kinamuwezesha kujitenga na imani potovu, mila ngumu na taasisi zinazotushikilia. Njia hiyo ni njia iongozayo kwa Mungu, kwa Mungu ndani mwetu.

S179SW • ISBN 978-3-96446-247-3 • Kurasa 76



Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mmekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake.

S170SW • ISBN 978-3-96446-226-8 • Kurasa 46



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu. Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha.

Ila, sala halisi, huhitaji mafunzo, kwa kuwa, sala halisi, tunayoifanya ndani mwetu wenyewe, ni mazungumzo na Mungu.

S174SW • ISBN 978-3-96446-225-1 • Kurasa 54



Amri Kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa

na kufafanuliwa katika usemi wa siku hizi, ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote.

S338SW • ISBN 978-3-96446-227-5 • Kurasa 46

Vitabu hivi vinapatikana pia katika lugha ya kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi pia

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
www.gabriele-publishing.com



Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany
www.gabriele-publishing.com